



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI MASASI
(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Unapojibu tafadhali taja:

MTC/L.10/IVOL VI/22

Tarehe: 06/03/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa zilizo rodheshwa katika tangazo hili kuomba nafasi ya kazi ya Udereva kama kibarua.

1. DEREVA DARAJA LA II - (Nafasi 3)

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na Cheti cha Awali cha Mafunzo ya Udereva na Cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka bila kusababisha ajali.

MAJUKUMU YA KAZI

- I. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- II. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- III. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- IV. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- V. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- VI. Kufanya usafi wa gari, na
- VII. Kufanya kazi nyingine kadri anavyoelekeza na Msimamizi wake.

POSHO.

Atakaye faulu usaili na kuajiliwa kama kibarua wa muda atalipwa posho ya shilingi 5000/= kwa siku.

MAELEKEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- A. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 18 na usiozidi 45.
- B. Maombi yaambatanishwe na taarifa ya maelezo binafsi (Curriculum Vitae) ya muombaji ikionesha wadhamini watatu na taarifa zao sahihi namba za simu za muombaji na wadhamini, cheti cha taaluma, cheti cha kidato cha nne, cheti

- cha kuzaliwa, na picha mbili passport size (ziandikwe majina kwa nyuma).
- C. Testimonial na provisional statemant of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita havitapokelewa.
- D. Muombaji atakaye wasilisha taarifa za kughushi au taarifa za Uongo kulingana na kiwango au sifa za kielimu na taaluma aliyonayo atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa taratibu.
- E. Baruaa zote ziandikwe kwa mkono kwa lugha ya kiswahili au kiingereza.
- F. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- G. Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili pia kupitia tovuti ya Halmashauri [www.masasitc go tz](http://www.masasitc.go.tz) pamoja na mbao za matangazo.
- H. Mwombaji awe na kitambulisho cha NIDA / Kitambulisho cha Mpiga Kura au namba ya usajili ya NIDA.
- I. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **10/03/2023** saa tisa na nusu (9:30 mchana).

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:
Mkurugenzi wa Mji,
S.L.P447,
MASASI.


ELIAS R. NTIRUHUNGWA
MKURUGENZI WA MJI
MASASI